# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**KABARAK HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

## KABARAK HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/3**

**Karatasi ya 3**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. **SHAIRI ( alama 20)**

- Ugumu wa maisha unaofananishwa na kufungwa kwa waya
- Hakuna mtu wa kumsaidia ila tu watazamaji wanamcheka
- Ukweli wa maisha umekuwa kama ndoto ya uwongo –alitarajia mema lakini umegeuka vitendawili
- Machozi na damu zinamtiririka bila wa kumhurumia na kumpanguza
- Babake ni mmoja wa wanaomcheka kisha anamsisitizia kwa atadondoka tu
- Vitumbo vimechongwa chini yake tayari kumtoboa
- Vichwa vimezuka ardhini –ishara ya wengi waliopitia njia hii gumu ya maisha Alama 4

2. Eleza kwa kutoa mifano miwili miwili jinsi msanii alivyotumia tamathali zifuatavyo: (al.6)

   - Jazanda
   - Tashihisi
   - Taswira
   - Jazanda

i) Vitimbo – Vikwazo katika maisha vinavyolemeza

ii) Waya – mhusika (binadamu )

iii) Kichomi –maisha magumu ya kukatisha tama

iv) Vichwa – Jazanda ya watangulizi wake waliopitia hali hii gumu.

(b) Tashihisi

- Kichwa kinasema kwa sauti
- Vitumbo vikingoja kumtoboa
- Vichwa vinacheka
- Kichomi kinampata

3. Andika ubeti wa saba kwa lugha tutuni (al 4)
   Mzunguzaji anasema kwamba sauti ya baba inamwarifu kwa kusisitiza kuwa hilo ndilo njia na ana nguvu lakini wakati utafika na atadondoka.Anaelezwa asitarajie msaada na sifa.Anaelezwa kuwa watangulizi wake walipita mkondo huo wa maisha.
4. Eleza maana ya mshororo "vichwa vyote hivi vilidondoka katika umbali uo, nawe kudondoka utadondoka" (al 2)
   Wengi wamepita matatizo / ugumu huo na huu mkondo wa maisha na ni lazima hayakumbali na kujizatiti.Mwisho ukifika ataondoka.
5. Eleza umbo la shairi hili (al 4)
   - Lina beti nane
   - Beti zote zina mishororo saba isipokuwa ubeti wa saba
   - Mishororo inatofuatiana, mingine mirefu na mingine mifupi.

   mfano ubeti 8 mshororo wa mwisho " kichomi kimenipata na sijaondoka"

   a) Halina mpangilio maalum wa vipandi

   b) Halina mtiririko wa vina.

2. a) Mktadha wa dondoo

- Dondoo hili lapatikana mwishoni mwa riwaya.
- Ni kauli ya Imani akimsemea Amani.
- Punde baada ya sherehe ya amu yake Amani kuachiliwa huru,Imani anamshajisha Amani kuandika tawasifu yake.
- Anamrai awasawiri vilivyo wanawake katika tawasifu ile. (alama 4*1=4)

b) Mbinu za uandishi.

- Nahau- usiniweke pembeni
- Tashbihi – kama tanbihi (Alama 2*1=2)

c) Usawiri wa Wahusika wa kike.

- Mwandishi ameweka sambamba wahusika hawa.
- Kuna wale wenye utu- Imani na Zuhura.
- Kuna wale wasio nao-Lowela,Michelle,na Mashaka.
- Walezi wema – Imani na Zuhura.
- Walezi wasio wema ni kama Lowela.
- Waadilifu kama Imani na mama yake.
- Wasio waadilifu kama Lowela.
- Wanaowajibika kazini kama imani na mama yake.

- Wa umri wa makamo kama Dora na Zuhura.
- Aidha kuna vijana kama Imani,Lowela na Mashaka.
- Jasiri- Imani na kwa kiwango fulani, Dora.
- Wengine wanaonekana kuishi kwenye vivuli vya wanaume (Hoja 7*2=14)

3. Katika nchi ya Tomoko, uhuru ni ndoto ambayo bado haijatimia. Jadili.

- Nchi ya Tomoko iliwahi kutawaliwa na waliodhulumu wenyeji – waliyatwaa mashamba yao, wakawakataza kufuga au kupanda mazao yaletayo fedha.Walishurutishwa kuwafanyia walowezi hawa kazi huku wakiishi katika mabanda. Walio mamlakani wanaendelea kuwadhulumu wanyonge.
- Waafrika walipochukua hatamu za uongozi mambo hayakubadilika . Walio mamalakani wanaendelea kuwadhulumu wanyonge.
- Mashamba yao yanatwaliwa mfano shamba la Chichiri na Mwinyihatibu.
- Wanafungwa jela kwa visingizo kama vile Yusuf na Amani.
- Vyombo vya Dora vinatumiwa kuendeleza matakwa ya watawala.
- Wanyonge wanafanyizwa kazi za kijungu jiko
- Lugha ya kikoloni ndiyo inayopendelewa nawatawala hawa weusi.
- Hawana uhuru wa kujiamulia mambo – Imani anatishwa na askari kwa kutohudhuria sherehe.Wananchi wamejazwa uoga.
- Ukosefu wa huduma muhimu kama vile matibabu.
- Uhuru wa kunena haupo mfano Matuko Weye anawekwa seli kwa kauli yake.
- Ukabila na ukoo unatumiwa katika kugawa nyadhifa na kazi – Nasaba Bora alipewa cheo cha utemi kwa upendeleo.
- Kitoto Uhuru ni ishara ya uhuru usio kamili , usiotunzwa na waliopewa jukumu la kuutunza.kufa kwake ni ishara ya utovu wa uhuru kamili.
- Ndoto huenda itatimia baada ya ukombozi wa pili ulioongozwa na Madhubuti na Amani.Madhila yatakomeshwa na haki kudumishwa. (Hoja zozote 10*2=20)

4. (a) Muktadha

   - Yalisemwa na mamake Dadavuo Kaole.

   - Alikuwa amweleza Daktari Siki.

   - Walikuwa hospitalini.

   - Hii ni baada ya mama kumpa mtotowe chakula cha mbwa kilichomfanya aendeshe.

   (b) Nidaa – si nyinyi nd'o mjuze wanangu!
   Mdokezo----nilikiona afadhali
   Lahaja- nd'o
   Tasifida- wanangu!

   (c) Uongozi mbaya

   - Migomo ya wafanyikazi.

   - Ukosefu wa vifaa muhimu vya kufanyia kazi.

   - Umaskini.

   - Udikteta.

- Ukosefu wa dawa.
- Mapuuza.
- Propaganda.

5.

a) Msemaji ni Diwani III✓ na alikuwa akimwambia Daktari Siki ✓nyumbani kwa Diwani III ✓alipomtembelea kutaka kujua hali ya mji wa Cheneo. Binamu yake Siki aliyeitwa Susi ambaye alikuwa Meya hakutaka kuelewa hali ya watu.Daktari alikuwa anataka Diwani III azungumze na Meya kuhusu ukosefu wa dawa hospitalini✓(asipotaja msemaji sufuri) (alama 4)

b) Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi. Kauli hii ina maana kwamba unapofanya jambo baya kimakosa hutarajii kupata mazuri baadaye. Watu walimchagua Meya ambaye alijaa ubinafsi, mwenye tama na katili. Meya huyo anawanyanyasa watu na kuwatesa . Alikataa kushughulikia maslahi ya wafanyakazi wa baraza la mji, kwa kuwa walichagua mtu asiyefaa isingewezekana kutarajia mema yoyote kutoka kwake. (Hoja zozote tatu, alama 6)

c) Kuna matendo mengi ya kuonyesha kuwa watu wa Cheneo walipanda pojo na kuvuna pojo si kunazi. Walichagua viongozi wabaya, waovu na hatima yake walivuna machungu ya uongozi mbaya.Meya alitoa kauli zozote kuwafurahisha watu Lakini hakutekeleza aliyoyasema. Alisema kuwa dawa zilikuwa njiani na zingefika baada ya siku tatu jambo ambalo halikuwa kweli.Hili ni tendo linaloonyesha uongozi mbaya.Alikuwa kinara wa baraza la mji na alikuwa na mamlaka ya kuamua mgao wa ardhi ya ummma.Alitumia nafasi hiyo vibaya kwa kunyakua vipande vinane vya ardhi na kumgawia rafiki ya Bili vine.Meya alitoa kandarasi kwa njia isiyofaa na aliposhitakiwa na mwanakandarasi wa zamani aliyepewa mkataba kisheria,Bili alimshawishi Meya kushirikiana na mwanakandarasi huyo ili kujipatia fidia kutoka katika baraza la mji na kisha wao kupata mgao wao.Meya alishirikiana na Bili, Diwani I na II kuuza fimbo ya Meya.Wafanyakazi waliogoma wakidai haki zao za; nyongeza ya mishahara, gharama kuwa ghali maishani , ukosefu wa dawa na mengineyo, walifurushwa vibaya na askari kwa amri ya Meya.Mji unachafuka na viongozi wa baraza chini ya Meya hawakujali kulishughulikia hilo.

d) Takriri -panda,vuna
Methali – mtu huvuna alichopanda. (Akataja ½, mifano ½)

**DAMU NYEUSI**

a) Ni maneno ya msimulizi.Anawaza haya baada ya kushindwa kumtoa ushamba mkewe.Ni baada ya kujipa moyo tena wa kutaka kumtoa kinyangaa.Aziza kwa kutaka kujua sababu yake kutovaa viatu nyumbani kwake.Hofu yake sasa ni kuwa hakutaka waliojifunga kuja kumtazama mke wangu namna alivyojirekebisha waondoke na zawadi za vichekesho. (al.4)

b)

| Msimulizi | Aziza |
|---|---|
| - Ni mbaguzi ambaye aliamini watu wa daraja la chini hawakupaswa kuchangamana na watu wa daraja la juu. | - Hana ubaguzi na alichangamana na kila mtu |

| | |
|---|---|
| - Anaathirika na tamaduni za kigeni na kupuuza tamaduni asilia | - Ni mwanajadi ambaye hataki kuathiriwa na usasa.Angali anang'ang'ana mambo ya jadi kama vile kutembea bila viatu. |
| - Anaathirika na elimu na utajiri katika familia<br>na kuzidharau kazi zingine hata | - Ni mkulima na mfanyikazi.Hili linadhibitika katika mikono yake ambayo imekomaa kutokana na kufanya kazi ngumu. |
| - Ni msomi na alizaliwa katika familia ya wakwasi | - Alitoka familia ya walala hoi na hakupata elimu yoyote. |

(Asipolinganisha mwanafunzi amekosea) (alama 8)

c)

- Kuchaguliwa mke. Kijana wa kiume katika jamii alioa kutokana na mke aliyechaguliwa na wazazi wake.
- Wana pia walilazimishwa kuoa au kuolewa wakishafika umri wa ndoa.

- Wanawake kudhunishwa kama vile kudai kuwa ndio wanaohitaji maongozi ya mume na si kinyume chake (al.6)

d)

- Mbinu zilizotumika
- Tashbihi
- Balagha (al.2)

6. Mke wangu

- kuchaguliwa mume
- Waliosoma na kwenda mijini kuchukuliwa kama wajuaji na kuharibika kimaadili.
- Anaonekana kuwa ndiye anayehitaji maongozi ya wanaume na si kinyume chake.
- Mke ndiye anayepaswa kustaarabishwa na mwanamume na si kinyume chake.

Maeko

- Mume amepewa haki ya kumpiga mkewe lakini mke hana ruhusa ya kumpiga mume.
- Mke anafanywa ngoma na pia kutusiwa vibaya.
- Kupigwa kwa wake haichukuliwi hatua yoyote ya kisheria.
- Hana usemi mbele ya mume.Anakesha kumngoja mume asijue anakotoka.
- Ni kiumbe duni mbele ya mwanamume.

Kanda la usufi

- Analaumiwa wana wanapokosa. Mama yake Sela analaumiwa pale Sela anapopata ujauzito.
- Sela anaposhika mimba anafukuzwa shuleni ilhali Masazu hakuathirika.
- Anatwikwa mzigo wa ulezi, mamake Sela ndiye anaonekana ana jukumu la kumlea mjukuu wake japo ni fukara.
- Mzee Butali ,baba yake Sela,anakasirika kuwafukuza mama na bintiye Sela.

**Mwana wa Darubini**

- Kubakwa na kulazimishwa kufanya mapenzi kinyume na matakwa yake kama vile kananda.
- Kunyang'wa mtoto kama vile kananda
- Kuchaguliwa ume-mwatela kumkabithi bwana mkongo kananda kama mke wake.
- Hana uwezo wa kufanya maamuzi apendavyo.
- Kananda anauzwa baada ya muda kama mtumwa na bwana Mkongo.

**Kikaza**

- Ni chanzo cha matatizo –Kuvunjwa kwa masharti ya kikazi katika jamii inatokana na Bi.Mtajika kuingiliamadaraka ya mumewe na kujifanya kiongozi.
- Wanabaguliwa na kunyimwa nafasi za uongozi.
- Kiumbe aliyejielewa na kuingilia wajibu usio wake kiasi kwamba akipewa fursa ya kusalimu wanakijiji
- anachukua saa nzima.
- Ni kiumbe cha kushangaza, kukasirisha na kuudhi. (zozote nne)

7.

a) Maghani –Ni ushairi ambao hutolewa kwa kalima badala ya kuimbwa.Hushughulikia maswali ya kijamii k.v kazi, maombolezi au siasa kama ilivyo katika nyimbo tofauti na nyimbo maghani hayaimbwi 2x1 = 2

b) Sifa za maghani

- Ni tungo za kishairi. Hii ina maana kuwa yana sifa za kishairi za kuwa na mapigo ya kimziki
- Husimulia matukio kwa kirefu hasa yanayotambwa.
- Hutungwa papo hapo na kusemwa au kutongelewa Mbele ya hadhira.
- Huweza kutolewa na mtu mmoja au kundi la watu.
- Huwa na majisifu ( majigambo)
- Huwa na uigizaji /utendaji
- Hutumia tamadhali za usemi kwa wingi

c)

- Kuandika
- Kunasa sauti – tepurekodi
- Kamera
- Video
- Sinema /filamu
- Akilini 4=Alama 4

d)

- Maandalizi- kuhusisha uteuzi wa mada, utambuzi wa malengo yaliyowazi katika mawanda ya

- utafiti,
- utambulizi wa mazingira na wakati ufaao na mbinu za ukusanyaji wa data.
- Ukusanyaji wa data yenyewe kwa kuhoji kushuhudia, kurekodi na hata kushirikisha.
- Kurekodi data kwa kuandika  kupiga chapa au video
- Kuchunguza data ili kutafsiri na kuandika upya neno kwa neno bila kupotosha maana ya lugha asili
- Kuchambua na kufasili data bila kupotosha maana
- Kuchambua na kufasili data ili kupata matokeo kamili ya utafiti

Hatua za mwanzo 5 x 1 =Alama

e)

- Ukosefu wa utafiti madhubuti
- Ukosefu wa walimu waalewa
- Vitabu virejelewa havipo
- Alama kuwa haina manufaa katika kuelimisha watu
- Baadhi ya vipera ni kinyume cha maadili ya kidini
- Vijana wa sasa hawaonei fasihi hii fahari
- Fasihi andishi yaelekea kuzingatiwa mno. zote 5 =Alama 5